**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**Simu Nam. + 255 24 2230602/1**
**Fax Nam. + 255 24 2230215**
**Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz**

**SANDUKU LA BARUA 902,**
**ZANZIBAR**
**Barua Pepe: zahore@zanlink.com**

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA BAJETI YA MWAKA 2021/2022

***Mheshimiwa Spika;*** Sina budi kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea na shughuli za Baraza.

***Mheshimiwa Spika;*** Pia, ninakushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako wote kwa kutuongoza vyema katika shughuli zetu za Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio waliotuwezesha kufika hapa kwenye chombo hiki adhimu.

***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uaminifu na uadilifu ili kuhakikisha kuwa mipango ya Serikali inatekelezwa kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi na kuimarisha maisha ya wananchi.

***Mheshimiwa Spika;*** Kamati inaomba kutoa shukrani zake za dhati kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Rahma Kassim Ali pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hii Ndugu Amour H. Bakari na wakurugenzi mbali mbali kwa juhudi zao na mashirikiano yao makubwa wanayoipatia Kamati yetu wakati wote wa kazi zake.

***Mheshimiwa Spika;*** Shukrani za pekee ziende kwa wajumbe wa Kamati hii ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kazi nzuri wanayoifanya katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa mnasaba huo, naomba sasa kuwatambulisha wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohammed Ahmada Salum Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Foum Mussa Mjumbe
4. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed (Mandoba) Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe Mjumbe
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo Mjumbe
7. Mhe. Ameir Abdulla Ameir Mjumbe

Aidha, Kamati hii ina makatibu wawili ambao nao hatuna budi kuwashukuru kwa kutekeleza majukumu yao kwa utaalamu na ufanisi mkubwa. Makatibu wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni, na
2. Ndg. Ali Alawy Ali.

***Mheshimiwa Spika;*** Baada ya utangulizi huo na kwa mujibu wa Kanuni ya 107(3) Jadweli la kwanza ambalo limetupa jukumu la kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kazi ambayo kwa kadiri ya uwezo wetu

tumejitahidi kuifanya kwa kufuatilia kiundani kabisa Utekelezaji wa Taasisi zote zilizochini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, katika vipindi tofauti ili kuhakikisha kuwa Dira na Malengo ya Serikali yanatekelezwa kwa kufuata Mipango ya Serikali, Ilani ya ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020/2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Sera ya Usafiri Zanzibar ya 2008.

***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi yenye **Fungu P 01** inatekeleza majukumu yake kwa kutumia Programu kuu *Tatu (3)* na Programu ndogo Nane (*8)* ambazo zinasimamiwa na Idara mbali mbali zilizochini ya Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea kama zilivyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

***Mheshimiwa Spika;*** Katika ***Program Kuu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji,*** Kamati inapongeza juhudi za Serikali kwa kuimarisha sekta ya usafirishaji kwa kujenga upya na kwa kiwango cha lami barabara mbali mbali mijini na vijijini. Katika utekelezaji wa program hii, Kamati inashauri kwamba barabara zote ambazo zimeanza kujengwa na zile zilizo katika mpango wa ujenzi kuzingatia kiwango cha ubora wa barabara hizo kwa kutumia wakandarasi wenye uzoefu kulingana na matumizi ya wakati huu ambapo teknolojia ya ujenzi imekuwa kwa kasi sana.

***Mheshimiwa Spika;*** Katika Programu Ndogo ya kwanza ya ***Usimamizi wa Usafirishaji:*** Kamati inashauri katika kudhibiti ajali Nchini kuvifanyia ukaguzi vyombo vya moto mara kwa mara na kuhakikisha madereva hasa wa gari za abiria na mizigo wanakidhi viwango kabla ya kupewa leseni. Aidha, Kamati inashauri

pia, kuangalia mifumo ya ulipaji leseni kwa njia ya mtandao ili ifanye kazi kwa ufanisi Zaidi.

***Mheshimiwa Spika;*** Katika uimarishaji wa Karakana Unguja na Pemba, Kamati inaupongeza Wakala wa Karakana Kuu ya magari hasa kwa upande wa Unguja kwa kufanya kazi kwa ufanisi baada kupatiwa vifaa vya kisasa, hivyo kwa kipindi kifupi kuyafanyia matengenezo magari yasiyopungua 900. Aidha, tunaomba Pemba pia, Karakana yao kuiangalia kwa jicho la huruma. Vile vile, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha wale wataalamu ambao wanahitaji sana katika baadhi ya vitengo kuwaombea ajira ili wapate kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Vile vile, Kamati inaitaka Wizara kufuatilia Fedha za Mapato zinazopatikana Karakana ili kurejeshwa asilimia yake pale zinapoenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, Kamati ilifika na kutembelea barabara ya Ole – Kengeja ambayo imekamilika kwa kiwango cha lami lakini bado kuna mambo ya msingi hayajakamilika kama vile alama za barabarani na misingi ya kutolea maji ya mvua. Kamati inaishauri Wizara kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli hizo baada ya kuarifiwa kuwa fedha zake zipo lakini bado hazijatumika kukamilisha kazi zilizobakia. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na ujenzi huo hasa maeneo ya mabondeni na miinuko kwa kujitokeza mipasuko kabla ya kukamilika kwake hivyo kupelekea kuwekewa viraka. Licha ya hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wakala wa Barabara kufanikisha ujenzi wa barabara hiyo ya kilomita 35.

***Mheshimiwa Spika;*** Sambamba na hayo, Kamati iliitembelea barabara ya Kipapo – Mgelema – Wambaa km 9.3 na kuridhishwa na kazi zinazoendelea licha ya changamoto ya vifaa na uhaba wa fedha, hivyo kupelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi huo. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kuingizia fedha

Wakala wa Barabara kwa ajili ya uendelezaji wa barabara hiyo muhimu kwa wananchi wa maeneo hayo ambayo yanazalisha kwa wingi zao la karafuu.

***Mheshimiwa Spika;*** Katika ziara mbali mbali za Kamati kwenye kufuatilia Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Bajeti ya 2020/2021, Kamati iligundua miradi kadhaa ya barabara ambayo ilitekelezwa na haijakamilika tofauti na mipango iliyokusudiwa. Hivyo, tunashauri Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia program ndogo ya "***Miundombinu ya Usafirishaji***" kukamilisha kwa haraka miradi yote ya barabara ambayo ilipangwa kukamilika ndani ya mwaka huu ili kuepusha gharama kwa Serikali, kwani kukaa muda mrefu barabara bila kuwekwa lami kunapelekea kuharibika kwa kifusi kilichowekwa, hivyo inagharimu tena Serikali kwa kuweka kifusi kipya wakati wa uwekaji lami.

***Mheshimiwa Spika;*** Kamati inashauri bajeti hii kuzingatia zaidi muendelezo wa miradi iliyoanzwa kutekelezwa badala ya kuanzisha miradi mipya ambayo itaithiri miradi ya nyuma isipokuwa kama Miradi hiyo itapata Wafadhili, miongoni mwa Miradi hiyo ni Jozani – Bwejuu kilomita 23, Kipapo – Mgelema kilomita 9.3 na Fuoni Daraja la Dkt Shein – Jumbi km 1.1, Finya – Kicha km 8.8 na Mradi wa ujenzi wa barabara ya Micheweni – Kiuyu Maziwa Ng'ombe kilomita 7.3

***Mheshimiwa Spika;*** Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali isaidie kukamilisha miradi hiyo kwa kuwapatia fedha za kutosha na kwa wakati ili kwenda sambamba na mipango ya barabara hizo. Aidha, Kamati inashauri kupitia barabara ya maeneo huru ya Micheweni, Pemba ambayo inajengwa kwa fedha za SMZ kazi ambazo zimeanza kutekelezwa zikamilike kwa wakati sambamba na

uwekaji wa lami, hata hivyo sehemu ya barabara ambayo imebakia kutoka Micheweni kuunganisha na barabara hii ni vyema ikafikiriwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuleta uwiano uliosawa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa barabara yote kwa ujumla.
Aidha, Kamati inashauri Barabara ya Fuoni – Tunguu kukamilishwa kwa sehemu iliyobaki kutiwa lami ngumu kwani imeshaanza kufanya mashimo na hivyo kupoteza taswira nzuri ya barabara hii.

***Mheshimiwa Spika;*** Kiujumla hali za barabara zetu kongwe nyingi haziridhishi na zaidi katika kipindi hiki cha mvua kutokana na kuwepo kwa mashimo makubwa yaliyosababishwa na maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba pamoja na changamoto ya upatikanaji wa lami kwa kipindi hiki; Kamati inashauri Wizara kufanya kila jitihada kuhakikisha barabara hizi zinarudi katika hali yake ya kawaida wakati mvua za masika zitakapo malizika ili kupunguza ajali za kizembe. Aidha, tunashauri barabara zote kuwa na misingi ya maji pale hali ya kifedha ikiruhusu ili barabara zidumu kwa muda mrefu.

***Mheshmiwa Spika;*** Kwa upande mwengine, Kamati imeridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) na hatua iliyobakia ni uwekaji wa mifumo ambayo itatumika katika kazi za kila siku. Kamati inashauri katika mpango wa ujenzi wa uzio pamoja na maegesho ya magari ukamilike kwa wakati ili uwanja huu uweze kukamilika na kwenda sambamba na soko la Dunia katika sekta ya Utalii. Aidha, Kamati inashauri Madawati ya kupokelea na kuondokea wageni pamoja na wafanyakazi wa Uhamiaji kuongezwa ili kuharakisha shughuli za kuhudumia Abiria. Pia, tunaipongeza Mamlaka kwa ukusanyaji mzuri wa mapato na tunawaomba waongeze kasi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya nane imedhamiria kutumia bandari kama mlango mkuu wa kukuza uchumi na kwa kuwa uchumi wa bluu ambao ndio shabaha kuu ya Serikali hauwezi kufikiwa bila ya kuwepo bandari za kisasa na zenye ufanisi. Kamati inashauri licha ya kuwepo kwa mpango mkubwa wa Serikali wa ujenzi wa bandari ya Manga Pwani na Mpiga Duri basi pia itumike juhudi ya pekee ya kuziimarisha bandari za zamani kama vile; bandari ya Mkokotoni ambayo ujenzi wake unaendelea, bandari ya Wete, bandari ya Wesha, bandari ya Mkoani na bandari ya Malindi.

***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, Kamati inalitaka Shirika la Bandari kusimamia kikamilifu ujenzi wa bandari ya Mkokotoni na kuhakikisha kwamba thamani halisi ya fedha imetumika katika ujenzi huo ambao asilimia hamsini ya fedha takribani bilioni 3 zimeshatolewa. Kamati pia, inatoa pongezi za dhati kwa Shirika la Bandari Zanzibar kwa hatua kubwa iliyofikiwa katika ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, Kamati inaliomba Shirika kuzidi kusimamia ukusanyaji wa mapato ili kuisadia Serikali kufikia malengo yake na kufanikisha Miradi ya Maendeleo iliyojiwekea ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kubebea makontena na mizani.

***Mheshimiwa Spika;*** Mamlaka ya Usafiri Baharini ni Sekta muhimu sana kwenye kuimarisha usafirishaji wa Abiria na mizigo. Kupitia Mamlaka hii sekta ya Usafirishaji Baharini, Vyombo vya Usafiri, Abiria na Mabaharia wote wako kwenye Mamlaka yao. Kamati inashauri zuio la usajili wa Meli za Nje ambalo limeathiri shughuli za Mamlaka kukusanya mapato kisheria kutatuliwa kwa haraka. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iangalie umuhimu wa kuanzisha chuo cha Mabaharia ili kuwasaidia vijana wetu wanaotaka kujiendeleza katika fani za Ubaharia kutokana na gharama kubwa zinazopatikana kupitia vyuo vya nje ya Zanzibar.

***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Shirika la Meli na Wakala wa Meli, Kamati pia inasikitishwa kwa Meli za MV. Mapinduzi II, MV. Maendeleo na Mt. Ukombozi II kutokufanya kazi zake kwa muda mrefu kutokana na matengenezo yake kuhitaji fedha nyingi ambazo Shirika halina uwezo huo.

Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia matengenezo Meli hizo na baadae kuzikodisha kama ilivyofanya kwa Meli yake ya mafuta ya Mt. Ukombozi.

***Mheshimiwa Spika;*** Program ya Pili ya *Miundombinu na Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano* (TEHAMA) kwa kuwa lengo kuu ni la programu hii ni kuhakikisha kuwepo kwa Miundombinu na huduma bora zenye kuendelea za TEHAMA, Kamati inashauri kuimarishwa kwa huduma hizo kwani zitasaidia sana kuimarisha ukushanyaji wa mapato kwa ufanisi na haraka.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano haukatwi mara kwa mara pale panapofanyika ujenzi wa barabara, upelekaji wa huduma za maji na umeme. Pia, Kamati inaikumbusha Serikali kuhusu ujenzi wa kituo kipya cha Taarifa (Data Centre) kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 – 2025. Pia, ufanyike Utaratibu wa kukiimarisha kituo kilichopo cha kuhifadhia Taarifa kutokana na mchango wake mkubwa kwenye Uchumi wa Zanzibar.

***Mheshimiwa Spika;*** Katika Program ya Uendeshaji na Uratibu ya Wizara: Kamati inashauri Wizara kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake wa kada tofauti ili kuwajengea uwezo. Aidha, Kamati inashauri fedha zilizopangwa kwa Idara ya Uendeshaji na Utumishi zipatikane kwa wakati. Kwa upande wa Idara ya Mipango, Kamati inashauri Wizara kusimamia na kuratibu vizuri Miradi mbali mbali ya Maendeleo ili ifanyike kwa viwango vinavyotakiwa na kwa kuzingatia thamani ya pesa (value for money).

***Mheshimiwa Spika;*** Katika suala la mapato, wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imepangiwa jumla ya Tsh bilioni 5.72 kwa mwaka 2021/2022 kwa kutegemea vyanzo vyake vya ukusanyaji wa mapato.

Wakati Kamati inapitia Kasma ya wizara hii ilibaini kwamba vyanzo vingi vya mapato vimewekewa makisio bila kuzingatia uhalisia wake katika ukusanyaji. Kamati inashauri wakati wizara inapangiwa mapato ufanyike utafiti wa kina ili kuona kama idara inayopangiwa kima fulani cha mapato upo uwezo wa kukusanya kiasi hicho na inadhibiti mapato hayo.

***Mheshimiwa Spika;*** Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ambapo wizara iliidhinishiwa jumla ya TSH: **177,410,373,000** na mpaka kufikia mwezi wa March 2021 Wizara imeingiziwa TSH: **48,332,675,936** sawa na asilimia **27.2** tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hali hii imepelekea Wizara kushindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.

***Mheshmiwa Spika;*** Aidha, Kamati imebaini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo imepungua kutoka **bilioni 177.4** mwaka jana hadi kufikia **bilioni 132.79** kwa mwaka 2021/2022. Kamati inashauri kutolewa ufafanuzi wa kina juu ya kupungua kwa fedha hizo za Miradi ya Maendeleo hasa kutoka Nje ambazo kwa mwaka huu ni Tsh **16,804,167,000.** Wakati fedha za Ndani ni Tsh **115,991,000,000.**

## HITIMISHO

***Mheshimiwa Spika;*** Kamati inashauri fedha zote ambazo zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ielekezwe katika miradi husika na

matumizi yake yafanyike kwa kuzingatia thamani ya fedha na mradi husika pamoja na kukamilisha miradi ambayo ilianza kutekelezwa katika Bajeti iliyotangulia.

***Mheshimiwa Spika;*** Mipango yote iliyomo katika Bajeti hii ya 2021/2022 haitoweza kutekelezeka ikiwa makusanyo ya mapato hayatafanyika kama ilivyokusudiwa kwa Taasisi zote ambazo zinahusika moja kwa moja na ukusanyaji wa mapato. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati kama zilivyopangwa kwenye Bajeti ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mwisho kabisa,** ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, kwa niaba ya Kamati yangu tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie kwa kina Bajeti hii na hatimae waidhinishiwe jumla ya fedha zote zilizopangwa kutumika kwa mwaka wa fedha *2021/2022* kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

***Mheshimiwa Spika;***

*Kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

**Ahsante,**

……………………………………

**(Mohammed Ahmada Salum)**

**Mwenyekiti,**

**KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**<u>ZANZIBAR</u>**